MWONGOZO RAHISI WA JUMUIYA ZA WATUMIAJI MAJI (WUA)

Kuimarisha Ushiriki wa Wanawake katika Uongozi na Maamuzi



Blue Victoria
For blue economy & thriving ecological biodiversity

LVBWB

IUCN

BRIDGE

YALIYOMO



Utangulizi 2

Malengo ya Mwongozo 3

Wigo wa Mwongozo 3

Maana ya Maneno Muhimu 4

Kazi za WUA 5

Ushiriki wa Wanawake Katika Uongozi na Ngazi za Maamuzi 5

Umuhimu wa Wanawake Kushiriki Katika Nafasi za Uongozi na Ngazi za Maamuzi Katia Jumuiya za Watumia Maji 6

Mwongozo wa Mikutano Shirikishi 8

Mpango wa Kukuza Wanawake Viongozi 9

Uhamasishaji wa Jamii 10

Mfumo wa Maamuzi Shirikishi 11

Njia za Kupokea Maoni 11

Hitimisho 12

1. UTANGULIZI



Mwongozo huu umeandaliwa kusaidia Jumuiya za Watumiaji Maji (WUA) kuboresha ushiriki wa wanawake katika uongozi na maamuzi yanayohusu matumizi, uhifadhi, na usimamizi wa rasilimali za maji. Wanawake ni watumiaji wakubwa wa maji katika kaya, kilimo, ufugaji, na shughuli za kiuchumi. Hata hivyo, mara nyingi hawashiriki kikamilifu katika nafasi za uongozi na maamuzi. Mwongozo huu unalenga kutoa mbinu rahisi na za vitendo kuhakikisha ushiriki wa usawa kwa maendeleo endelevu ya jamii.

1.1 MALENGO YA MWONGOZO

- Kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi wa WUA na jamii
- Kuimarisha maamuzi shirikishi katika usimamizi wa rasilimali maji
- Kuboresha uwajibikaji na usimamizi wa rasilimali za maji
- Kukuza usawa wa kijinsia katika jamii.
- Vyama vya watuamiaji maji lazima ziangalie uwiano wa kijinsia katika kamati tendaji
- Pale ambapo hili haliwezekaniki kutekelezwa, hatua za utekelezaji wa taratibu zinapaswa kubainishwa (kwa mfano kutenga viti maalum au nafasi za unaibu)

1.2 WIGO WA MWONGOZO

Mwongozo huu unatumika kwa:

- Jumuiya za Watumiaji Maji (WUA)
- Serikali za vijiji
- Kamati za maji
- Wadau wa maendeleo.



2. MAANA YA MANENO MUHIMU



WUA ni nini?

WUA ni kifupi cha maneno Water User Association yaani Jumuiya ya Watumia Maji. Hiki ni kikundi cha watumiaji wa maji kutoka chanzo kimoja wanaoshirikiana kusimamia matumizi ya maji kwa uendelevu.

Jinsia ni nini?

Jinsia ni nafasi, majukumu na matarajio ambayo jamii huweka kwa wanawake na wanaume. Mfano: wanawake hutegemewa kutafuta maji na kutunza familia, wakati wanaume mara nyingi huongoza vikao.

Usawa wa Kijinsia

Ni hali ambapo wanawake na wanaume wanapata nafasi sawa katika maamuzi, uongozi, elimu, na fursa za maendeleo.

Uongozi wa Wanawake

Ni wanawake kushiriki katika nafasi za maamuzi kama mwenyekiti, katibu, mweka hazina, au mjumbe wa kamati.

Ushirikishwaji katika Maamuzi

Ni kuhakikisha kila mtu hasa wanawake, vijana, na makundi maalum anapata nafasi ya kutoa maoni na kushiriki katika maamuzi.

3. KAZI ZA WUA

- Kusimamia matumizi ya maji kwa haki na uendelevu
- Kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji (mito, chemchemi, visima)
- Kutatua migogoro ya maji
- Kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi bora ya maji
- Kuhakikisha ushiriki wa wanawake, vijana, na makundi maalum
- Kushirikiana na serikali na wadau wengine katika kuendeleza Rasilimali za maji.

4. USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA UONGOZI NA NGAZI ZA MAAMUZI

Lengo

Kuangalia kama wanawake wanashiriki kweli katika uongozi na maamuzi Katika jumuiya za watumia maji (WUA).

Mambo ya Kuangalia

Uongozi

- Je, wanawake ni angalau asilimia 40-50 katika viongozi?
- Je, wanawake wapo kwenye kamati muhimu?
- Je, wanawake wanapewa nafasi za juu kama mwenyekiti au katibu?
- Je, wanawake wanashiriki katika usimamizi wa bajeti, utekelezaji wa kanuni/sheria, au utatuzi wa migogoro- na siyo katika majukumu ya kijamii?

Ushiriki wa Vikao

- Je, wanawake wanahudhuria mikutano?
- Je, wanawake wanapewa nafasi ya kuzungumza?
- Je, maoni yao yanazingatiwa?
- Je, mapendekezo yaliyotolewa na wanawake yanazingatiwa na kujumuishwa katika maamuzi ya mwisho?

Mazingira Salama

- Mikutano inafanyika muda unaowafaa wanawake?
- Hakuna vitisho au kubezwa?
- Eneo la mkutano ni salama?

5. UMUHIMU WA WANAWAKE KUSHIRIKI KATIKA NAFASI ZA UONGOZI NA NGAZI ZA MAAMUZI KATIKA JUMUIYA ZA WATUMIA MAJI

Wanawake ni watumiaji wakubwa wa maji katika familia, kilimo, ufugaji, biashara ndogo ndogo, na shughuli nyingi za kila siku. Wanahusika moja kwa moja katika kutafuta, kutumia, na kuhifadhi maji, hivyo wana uelewa mkubwa wa changamoto zinazohusiana na upatikanaji wa maji. Kushiriki kwa wanawake katika nafasi za uongozi na ngazi za maamuzi ndani ya Jumuiya za Watumia Maji (WUA) ni muhimu kwa sababu zifuatazo:

i.Huleta Maamuzi bora na yenye uhalisia
Wanawake wana uzoefu wa moja kwa moja kuhusu matumizi ya maji katika maisha ya kila siku. Ushiriki wao husaidia maamuzi kufanyika kwa kuzingatia mahitaji halisi ya familia na jamii.

ii. Huongeza Usawa na Haki
Wanawake wanapopata nafasi ya kushiriki katika maamuzi, kunakuwa na usawa wa kijinsia na haki katika ugawaji wa rasilimali za maji, huduma, na fursa za maendeleo.

iii. Huboresha Usimamizi wa Rasilimali za Maji
Wanawake mara nyingi ni walinzi wa matumizi ya maji nyumbani na shambani. Wakiwa viongozi, wanaweza kusaidia kuimarisha uhifadhi wa maji, matumizi bora, na ulinzi wa vyanzo vya maji.

iv. Hupunguza Migogoro ya Maji
Wanawake wana uwezo mkubwa wa kujenga maelewano na kutatua migogoro kwa njia ya mazungumzo. Ushiriki wao unaweza kusaidia kupunguza migogoro ya matumizi ya maji katika jamii.

v. Hupunguza Migogoro ya Maji
Wanawake wana uwezo mkubwa wa kujenga maelewano na kutatua migogoro kwa njia ya mazungumzo. Ushiriki wao unaweza kusaidia kupunguza migogoro ya matumizi ya maji katika jamii.

Vi. Huongeza Uwajibikaji na Uwazi
Wanawake wengi wanapopewa nafasi ya uongozi, mara nyingi huleta uwajibikaji mkubwa, usimamizi mzuri wa rasilimali, na uwazi katika maamuzi ya jumuiya.

Vii. Kupata nafasi za uongozi huwasaidia wanawake kujenga uwezo wa kujieleza, kufanya maamuzi, na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii.

Viii. Huchochea Maendeleo ya Jamii Nzima
Jamii inapowashirikisha wanawake na wanaume kwa usawa, maendeleo huwa ya haraka, endelevu, na yenye manufaa kwa kila mtu.

6. MWONGOZO WA MIKUTANO SHIRIKISHI

Kabla ya mkutano

- Toa taarifa mapema
- Tuma mwaliko kwa wanawake moja kwa moja
- Chagua muda unaofaa
- Hakikisha agenda zinaeleweka.

Wakati wa mkutano

- Ruhusu kila mtu kuzungumza
- Tumia vikundi vidogo inapobidi kama wanawake wanaona aibu
- Uliza mwanamke mmoja mmoja kutoa maoni
- Heshimu mawazo ya wote.

Baada ya mkutano

- Andika maamuzi
- Fuatilia utekelezaji
- Kusanya maoni.

7. MPANGO WA KUKUZA VIONGOZI WANAWAKE

- Tambua wanawake wenye uwezo
- Wape mafunzo ya uongozi
- Wape nafasi za kuongoza
- Wape ushauri na uongozi.

Jua mahitaji yao.
Wanahitaji nini?

- Ujasiri wa kuzungumza
- Elimu ya uongozi
- Maarifa ya usimamizi wa maji
- Uwezo wa kusimamia migogoro

Wape nafasi

- Waongoze kikao kidogo
- Wawe viongozi wa kamati
- Wawakilishe WUA kwenye mikutano ya nje

Wape ushauri

Waunganishe na viongozi wenye uzoefu.

8. UHAMASISHAJI WA JAMII

Wanawake mara nyingi hukumbana na changamoto nyingi zinazozuia ushiriki wao katika usimamizi na utawala wa rasilimali za maji.

Vikwazo vya kawaida vinavyoathiri uongozi wa wanawake

- Mzigo mkubwa wa kazi za malezi na utunzaji zisizolipwa pamoja na jukumu la kutafuta na kuchota maji
- Kiwango cha chini cha elimu au ujuzi wa kusoma na kuandika
- Mila na desturi zinazowazuia wanawake kuzungumza na kutoa maoni hadharani
- Kukosa upatikanaji wa taarifa muhimu au mitandao ya kijamii ma kitaaluma inayoweza kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika maamuzi.

Lengo

Kupunguza upinzani dhidi ya wanawake viongozi na kuongeza uelewa wa jamii.

Ujumbe Muhimu

- Wanawake ni watumiaji wakubwa wa maji
- Wanawake wakishirikishwa maamuzi, huduma huwa bora
- Uongozi wa wanawake unasaidia familia na jamii
- Kuwashirikisha viongozi na wanachama wanaume kuwa mabalozi wa usawa wa kijinsia
- Kuhamasisha mgawanyo wa majukumu nyumbani kati ya wanaume na wanawake ili wanawake waweze kupata muda wa kuhudhuria mikutano.

Njia za Kutumia

- Mikutano ya kijiji
- Majadiliano ya jamii
- Ushuhuda wa wanawake
- Vikundi vya vijana
- Ushirikishwaji wa wazee na viongozi wa dini.

9. MFUMO WA MAAMUZI SHIRIKISHI

Hatua 5

1. Tambua Tatizo

Mfano: upungufu wa maji au mgogoro wa matumizi ya maji.

2. Kusanya Maoni

Pata maoni kutoka kwa wanawake, wanaume, vijana, na viongozi.

3. Jadili Suluhisho

Linganisha njia mbalimbali za kutatua tatizo.

4. Fanya Uamuzi

Tumia makubaliano au kura ya wazi.

5. Andika na Taarifu

Andika maamuzi na wajibu wa kila mtu.

10. NJIA ZA KUPOKEA MAONI

Lengo

Kutoa nafasi salama kwa wanawake na wanachama
kutoa maoni, malalamiko, au mapendekezo, kwakukomesha au kukatisha tamaa unyanyasaji, kejeli au adhabu dhidi ya viongozi wanawake.

Njia

- Utaratibu rahisi wa kuripoti na kushughulikia malalamiko unapaswa kuandaliwa na kutekelezwa
- Vikao vya wanawake pekee
- Simu
- Mtu wa kuaminika wa kupokea maoni

Muhimu

- Siri ihifadhiwe
- Maoni yashughulikiwe
- Wanachama wajulishwe hatua zilizochukuliwa

11. UWAJIBIKAJI NA UFUATILIAJI

Sehemu hii inalenga kufuatilia maeendeleo ya matokeo ya kijinzia,zaidi ya maoni baada ya utekelezaji

Viashiria vinavyozingatia usawa wa kijinsia.

- % ya wanawake katika nafasi za uongozi kwenye kamati tendaji
- % mikutano ambapo wanawake ushiriki kikamilifu kwa kutoa maoni
- Idadi ya maamuzi yanayopendekezwa na wanawake ambayo yanakubaliwa/kutekelezwa
- Uwepo wa angalau mwanamke mmoja kama mtia saini katika akaunti za fe

12. HITIMISHO

WUA yenye wanawake wanaoshiriki kikamilifu huwa na maamuzi bora, uwajibikaji mkubwa, na usimamizi mzuri wa maji. Kumpa mwanamke nafasi ya uongozi si upendeleo bali ni njia ya kuimarisha msingi wa maendeleo endelevu ya jamii.



Mwongozo huu umeandaliwa na Shirika la Blue Victoria kwa Kushirikiana na Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria- Dakio la Mto Mara, kwa udhamini wa shirika la International Union for Conservation of Nature (IUCN)